




**Learning on TAP**

# Teknolojia saidizi
## Maneno muhimu: Vifaa saidizi vya usikivu

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Kifaa saidizi cha usikivu kinachowekwa nyuma ya sikio (BTE)** | Aina ya kifaa saidizi kinachowekwa nyuma ya sikio la mtumiaji. |  |
| **Kipandikizi cha koklea** | Ni kipandikizi cha kielektroniki ambacho kinasaidia mtu aliyepoteza usikivu kwa **kiwango kikubwa** hadi **kikubwa zaidi** ( mtu ambaye ni kiziwi). Kinakuwa na sehemu nya ndani ( iliyopandikizwa) na kifaa cha kuchakata kinachowekwa kwa nje). |  |
| **Kiziwi** | Ni neno linalotumika kuonyesha upotevu wa kusikia kwa kiwango **kikubwa** hadi **kikubwa zaidi** kwa masikio yote mawili kwa vile mtu mwenye tatizo hilo anaweza kusikia tu sauti kubwa mno au kutokusikia kabisa. Watu ambao ni viziwi wanawekewa vipandikizi vya koklea au wanatumia lugha ya alama kwa mawasiliano. | |
| **Kutokwa na uchafu** | Majimaji yanayotoka sehemu ya mwili. Mara nyingi kitendo hiki ni dalili ya maambukizi. |  |
| **Mtaalamu wa masikio na usikivu** | Wataalamu ambao hupima, kudhibiti na kutibu matatizo ya masikio na usikivu | |
| **Mfereji wa sikio** | Sehemu ya nje ya sikio ambayo inaanzia kwenye pina hadi kwenye ngoma ya sikio |   |
| **Ngoma ya sikio (utando wa timpaniki)** | Utepe mwembamba ambao unatenganisha sehemu ya nje ya sikio, sehemu ya kati ya sikio na unalinda sehemu ya kati ya sikio dhidi ya maambukizi. |   |

| | | |
|---|---|---|
| **Kitu kutoka nje ya mwili** | Ni kitu kisichotakiwa ambacho kimenasa kwenye sehemu ya mwili ambapo hakistahili kuwepo. Kwa mfano, punje ya udongo ilinasa kwenye ukope au mdudu aliyenasa kwenye mfereji wa sikio. |  |
| **Shida katika kusikia** | Neno linalotumika kwa mtu aliyepoteza usikivu kwa **kiasi kidogo** hadi **kikubwa**, ambaye hawezi kusikia vizuri kama mtu aliye na usikivu wa kawaida. | |
| **Otoskopu** | Kifaa kuza chenye mwanga ambao unatumika kukagua kwa macho sikio la mtu anayefanyiwa kipimo. |  |
| **Pina** | Sehemu ya nje ya sikio inayoonekana. |  |
| **Kifaa saidizi cha usikivu kilichosetiwa tayari** | Ni aina ya kifaa saidizi ambacho tayari kimesetiwa kwendana na aina za upotevu wa usikivu uliozoeleka. | |
| **Kifaa saidizi cha usikivu kinachoweza kusetiwa** | Ni aina ya kifaa saidizi cha usikivu kinachoweza kusetiwa ili kwendana na mahitaji maalumu ya mhusika. | |
| **Usaha** | Ni ute mzito unaotokea pale mwili unapopambana na maambukizi. Yawezekana ukawa na rangi au harufu isiyo ya kawaida. | |
| **Speculumu** | Sehemu ya juu ya Otoskopu inayoweza kuondolewa, ambayo huingizwa ndani ya sikio la mtu anayepimwa. |  |
| **Tragusi** | Sehemu ya pina inayofunika na kulinda mlango wa mfereji wa sikio. |   |
| **Utambi** | Ni kipande cha kitambaa/karatasi kinachotumika kufyonza majimaji. |  |